Ref: PAP.5/PLN/RES/1-7/OCT.19
Original: English

BUNGE LA TANO

Mkutano wa Tatu wa Kawaida

Tarehe 6 hadi 18 Oktoba 2019

# MAAZIMIO

*Kaulimbiu ya mwaka 2019: "Mwaka wa Wakimbizi, Wanaorejea makwao na Wakimbizi wa Ndani: Mchango wa Bunge la Afrika Kuelekea Kupata Suluhisho la Kudumu la Uhamiaji wa kulazimishwa barani Afrika"*

PAP.5/PLN/RES/1/OCT.19

**AZIMIO LA KUANZISHA UPITISHAJI WA SHERIA YA MFANO YA ULEMAVU KATIKA AFRIKA**

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha "ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara";

**LIKIZINGATIA PIA**, Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, inayolipa BA mamlaka ya kuwezesha ushirikiano wa kanda, maendeleo na uhimizaji wa "kujitegemea kwa pamoja na kufufua uchumi" wa Umoja wa Afrika;

**LIKIZINGATIA ZAIDI** Ibara ya 11 (3) ya Protokali ya BA na Kanuni ya 4 (1) (d) & (e) ya Kanuni za Uendeshaji wa BA, ambayo inalipa BA mamlaka ya kufanya kazi ya uoanishaji au uratibu wa sheria za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, pamoja na mambo mengine, kupitia kupendekeza na kuandaa sheria za mfano;

**LIKIZINGATIA ZAIDI** Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za watu wenye Ulemavu, na na katika kutumia njia mifumo ya kijamii na kitababu, ambazo zinahakikisha haki sawa kwa watu bila kujali hali zao, ikiwemo ulemavu;

**LIKIKUMBUKA ZAIDI**, Azimio la BA kuhusu Sheria ya Mfano ya Ulemavu barani Afrika, ambalo lilipitishwa wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Tano, mwezi Oktoba 2018;

**LIKITAMBUA** kwamba watu wenye ulemavu wanakabiliwa na ubaguzi na vikwazo ambavyo vinawazuia kushiriki katika maisha ya kijamii kwa usawa na wengine, wananyimwa haki zao za kuishi kwa uhuru katika jamii pamoja na ulinzi wa kijamii;

**LIKIKARIBISHA** ushirikiano kati ya Bunge la Afrika na Muungano wa Watu wenye Ulemavu Afrika katika kutimiza haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu kwa kukuza na kujumuisha ulemavu ndani ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kupitia uandaaji wa Sheria ya Mfano ya Ulemavu;

**LIKITHAMINI** michango kutokana na mashauriano ya kanda kuhusu Rasimu ya Sheria ya Mfano ya Ulemavu ambayo inatoa fursa kwa raia wa Afrika, mashirika ya ngazi ya chini na wadau wengine wenye nia kujihusisha na rasimu ya Sheria ya Mfano;

**LIKITHAMINI PIA** pia msaada wa kitaalamu uliotolewa na Muungano wa Watu wenye Ulemavu Afrika kwa Bunge la Afrika katika kuandaa na kushauriana kuhusu rasimu ya sheria ya mfano ya ulemavu, ambayo itawezesha kutumika katika nchi kwa Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusiana na Haki za Watu wenye Ulemavu pamoja na kutunga sera na sheria za taifa za haki za binadamu kuusu ulemavu;

**LIKIAMINI** kwamba mfumo wa sheria wa ara ulio kamili na jumuishi wa kusaidia kukuza na kulinda haki za watu wenye ulemavu utatoa mchango mkubwa katika kurekebisha udhaifu mkubwa wa mazingira magumu ya kijamii ya watu wenye ulemavu na kukuza ushiriki wao katika nyanja za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kuitamaduni, katika ngazi zote za kitaifa na kimataifa;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. **KUPITISHA** Sheria ya Mfano ya Ulemavu;

2. **LINAOMBA** Uongozi wa BA kuwasilisha Sheria ya Mfano ya Ulemavu kwa Vyombo vya Sera vya UA kwa ajili ya kuidhinishwa na kutumiwa na Nchi Wanachama wa UA.

3. **KUTEKELEZA** shughuli za uhamasishaji kwa ajili ya uridhiaji wa Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu unaohusiana na Haki za Watu wenye Ulemavu na kuidhinishwa na kutumiwa na Nchi Wanachama wa UA;

4. **KUIMARISHA** ushirikiano na kujadiiana kati ya bunge za kanda na kitaifa, kwa lengo la kuongeza uwezo wa wabunge wa kufuatilia na kukuza ujumuishaji wa ulemavu katika sera na mipango ya kitaifa, pamoja na vyombo vya bajeti na sheria.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

**PAP.5/PLN/RES/2/OCT.19**

## AZIMIO KUHUSU SHERIA YA MFANO YA USALAMA WA CHAKULA NA LISHE AFRIKA

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha "ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara";

**LIKIZINGATIA** pia Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, inayolipa BA mamlaka ya kuwezesha ushirikiano wa kanda, maendeleo na uuhimizaji wa "kujitegemea kwa pamoja na kufufua uchumi" wa Umoja wa Afrika;

**LIKIZINGATIA ZAIDI** Ibara ya 11 (3) ya Protokali ya BA na Kanuni ya 4 (1) (d) & (e) ya Kanuni za Uendeshaji wa BA, ambayo inalipa BA mamlaka ya kufanya kazi ya uoanishaji au uratibu wa sheria za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, pamoja na mambo mengine, kupitia kupendekeza na kuandaa sheria za mfano;

**LIKIKUMBUKA** Azimio la BA kuhusu kuandaa Sheria ya Mfano ya Usalama wa Chakula na Lishe katika Afrika, ambalo lilipitishwa wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Tano, mwezi Oktoba 2018;

**LIKITAMBUA** kwamba nchi nyingi za Afrika ni wadau katika mikakaba ya kimataifa inayohusu usalama wa chakula na lishe (FSN), kama vile Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Uchumi, Jamii na Utamaduni, na kwamba haki ya chakula cha kutosha imeelezwa wazi katika Katiba za Kitaifa za nchi nyingi barani Afrika;

**LIKIZINGATIA** kwamba sera na mifumo ya FSN iliyowekwa katika sheria inafaa zaidi na inakuza uboreshaji endelevu wa FSN, na umuhimu wa kushughulikia changamoto za kimuundo, sera maalumu, programu, sheria na mazingira ya kuwezesha FSN;

**LIKIZINGATIA** uwasilishaji wa rasimu ya Sheria ya Mfano ya Usalama wa Chakula na Lishe, ambayo inazingatia hali mtambuka na ya sekta mbalimbali ya FSN na mitazamo tofauti ya utaratibu wa kisheria za Mataifa ya Afrika;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. **KURIDHIA** rasimu ya kwanza ya Sheria ya Mfano ya FSN barani Afrika;

2. **KUIOMBA** Kamati ya Kilimo kufanya mashauriano ya kikanda kuhusu Rasimu ya Sheria ya Mfano ya FSN katika Afrika, ili kuunganisha michango kutoka kwa raia wa Afrika, mashirika ya ngazi ya chini na wadau wengine wenye nia;

3. Inakaribisha msaada wa kitaalamu kutoka FAO na ushirikiano wenye manufaa kati ya PAPA-FSN, Kamati ya Uchumi Vijijini, Kilimo, Maliasili na Mazingira, Ushirikiano mpya wa Shirika la Maendeleo Afrika (NEPAD), na Idara ya Kamisheni ya Uchumi Vijijini Afrika na Kilimo, kwa uandaaji wa Rasimu ya Sheria ya Mfano ya FSN.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

**AZIMIO LA KUANZISHA JUKWAA LA ELIMU LA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA**

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA** pia Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, inayolipa BA mamlaka ya kuwezesha utekelezaji wa sera, malengo na programu za Umoja wa Afrika na kusimamia utekelezaji wake mzuri;

**LIKIREJEA** Uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA, mwezi Julai 2004, ambalo ulianzisha, Kituo cha Kimataifa cha Elimu ya Wasichana na Wanawake Barani Afrika (AU / CIEFFA), kama taasisi ya kukuza elimu ya wasichana na wanawake katika Afrika;

**LIKIREJEA PIA** mapendekezo ya Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Umoja wa Afrika katika mkutano wao wa pili uliofanyika huko Algiers mwezi Aprili 2005 kuhusu kuanzisha Taasisi ya Kiafrika ya Elimu ya Sayansi kwa Maendeleo (IPED) kama taasisi maalumu ya UA yenye jukumu ya kufanya kazi kama Mwangalizi wa Elimu ya Afrika kwa lengo la kukuza maendeleo ya elimu bora, inayosaidia na jumuishi barani Afrika kwa kuhakikisha Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Elimi (EMIS) wenye nguvu na unaofanya kazi na mipango mizuri ya maarifa;

**LIKIREJEA ZAIDI** Uamuzi uliopitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA, mwezi Julai, 2010, wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Afrika, ambacho kinalenga kufufua elimu ya juu na Utafiti katika Afrika kwa lengo la kuongeza ubora wa elimu ya sayansi;

**LIKIZINGATIA** kwamba Mkakati wa UA wa Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kwa Afrika 2024 (STISA-2024) unaweka sayansi, teknolojia na uvumbuzi katika kitovu cha maendeleo na ukuaji wa kiuchumi na kijamii wa Afrika na inasisitiza matokeo yanayoweza kuletwa na sayansi katika sekta muhimu kama za kilimo, nishati, mazingira, afya, maendeleo ya miundombinu, madini, usalama na maji mingoni mwa sekta nyingine.

**LIKIZINGATIA PIA** umuhimu wa jukumu linalofanywa na elimu katika kufanikisha Lengo la Ajenda ya 2063 na kufuatia mahitaji ya Afrika kufanya uwekezaji mkubwa katika kukuza mtaji wa binadamu na jamii kupitia elimu na ustadi unaosisitiza uvumbuzi, sayansi na teknolojia;

**LIKIREJEA** Mkakati wa Elimu ya Bara kwa Afrika (2016/2025) uliopitishwa na Mkutano wa 26 wa Kawaida wa Baraza la Utendaji la UA, ambao umetoa wito wa utashi wa kisiasa

wa pamoja katika kuanzisha mageuzi ya elimu ili kubadilisha mifumo ya elimu na mafunzo ya Afrika ili kukudhi maarifa, uwezo, ustadi, uvumbuzi na ubunifu unaohitajika kukuza maadili ya msingi ya Afrika na kuhimiza maendeleo endelevu katika ngazi ya taifa, kanda ndogo na bara;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. Kuanzisha Jukwaa la Elimu la Wabunge wa Bunge la Afrika (PAP-FED) kama ifuatayo:

   1.1. PAP-FEB litakuwa na malengo yafuatayo:

      a. Kujitahidi kuwahamasisha wabunge kuzidisha maendeleo katika elimu;

      b. Kuimarisha jukumu la wabunge katika kuandaa mifumo na nyaraka za kisheria kwa ajili ya kuendeleza elimu katika ngazi ya taifa, kanda na bara;

      c. Kushiriki katika mchakato wa kufuatilia utekelezaji wa mikakati, sera na miradi ambayo makubaliano yalifikiwa kuhusu kuendeleza elimu katika Afrika;

      d. Kuwa na mazungumzo ya kujenga na uvumbuzi wa pamoja kati ya wabunge na wadau wote katika elimu kuhusu mitaala na programu za mafunzo kwa maendeleo ya binadamu, kushirikiana vyema na wataalamu wa elimu katika nchi zote kwenye bara hili ili kuboresha mahali pa elimu katika jamii katika ngazi za kanda na bara;

      e. Kuunga mkono ushirikiano kati ya wabunge wa mabunge yote ya Afrika ili kutengeneza mfumo wa kisheria wa kurejewa na bara la Afrika ili kupata fursa sawa za elimu kwa wote na kuhakikisha kuwepo kwa elimu bora;

      f. Kutengeneza mifumo ya kisheria ya bara kuhusu elimu ili kuendeleza utoaji wa fursa za elimu na kupunguza idadi ya wanaoacha shule katika ngazi zote za elimu katika Afrika;

      g. Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya elimu, miradi na sera ili kuhakikishi kuwa watoto wote wa shule wanajumuishwa kikamilifu katika mizunguko

mbalimbali na pia kutoa elimu na mafunzo kwa watu wazima, ili kumaliza suala la kuacha shule na kuzuia kuenea kwa hali ya kutojua kusoma na kuandika kwa kutumia mbinu za kisasa za kujifunza.

1.2. Kamati ya Utendaji ya PAP-FED chini ya usimamizi wa Kamati ya Elimu, Utamaduni, Utalii na Rasilimali Watu, itakuwa na wajumbe wa Kamati ya Elimu, Utamaduni, Utalii na Rasilimali Watu pamoja na wajumbe wa kamati nyingine za BA zinazohusika.

1.3. PAP-FEB itafanya mikutano yake ya mwaka katika miji mikuu mbalimbali ya Afrika ili kuhakikisha:

a. kuwepo kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa utekelezaji wa uamuzi unaohusu elimu katika bara la Afrika;

b. kufaidika na masuluhisho ya kielimu na uzoefu wa nchi tofauti ili kufikia malengo yanayohitajika.

2. Kuwaalika wabunge wote wa kitaifa, kikanda na kimataifa, na wadau wengine muhimu, kuteua wawakilishi wao kwenye PAP-FED;

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

**AZIMIO LA KUPITISHA MAKUBALIANO YA SHERIA YA MFANO YA UTOZAJI KODI MARA MBILI**

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA** pia Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, inayolipa BA mamlaka ya kuwezesha utekelezaji wa sera, malengo na programu za Umoja wa Afrika na kusimamia utekelezaji wake mzuri;

**LIKIREJEA** Azimio Maalum la Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa UA kuhusu Usafirishaji Haramu wa Fedha kwenye Mkutano wa Kawaida wa Ishirini na Nne huko Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Januari 2015 na Mapendekezo ya Ripoti ya Jopo la Viongozi kuhusu Usafirishaji Haramu wa Fedha kutoka Afrika;

**LIKIREJEA PIA** Azimio PAP.5/PLN/RES/10/MAY.19 kuhusu Uandaaji wa Makubaliano ya Mfano wa Utozaji Kodi Mara Mbili Afrika, yaliyopitishwa na Bunge la Afrika tarehe7 Mei, 2019;

**LIKIZINGATIA** hatua iliyofikiwa na Kamati ya Fedha katika utekelezaji wa Azimio lililotajwa hapo juu, shukrani kwa ushirikiano wenye mafanikio na Jukwaa la Usimamizi wa Kodi Afrika (ATAF), Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) na Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuhusu Sheria za Kimataifa (AUCIL);

**LIKISISITIZA** umuhimu wa nchi za Afrika kuwa na utaratibu thabiti na uliyooanishwa katika mazungumzo yao ya utozaji kodi, ambao utaendeleza uhakika wa ongezeko la kodi na mazingira bora ya uwekezaji na biashara;

**LIKISISITIZA ZAIDI** kwamba Makubaliano ya Mfano wa Utozaji Kodi Mara Mbili yanaweza kuwa nyenzo inayofaa ya kukuza biashara na uwekezaji ulio sawa miongoni mwa Mataifa ya Afrika na yasiyo Mataifa ya Kiafrika, na kuwezesha utekelezaji wa uamuzi wa UA wa kukomesha Usafirishaji Haramu wa Fedha kutoka Afrika na shughulikia mapato ya chini ya kodi za makampuni ambayo husababisha mfumo wa kodi usio sawa na mapato ya chini ya kodi katika bara;

**LIKITHAMINI** michango ya mashauriano ya kitaalamu kuhusu Rasimu ya Makubaliano ya Utozaji Kodi Mara Mbili, ambayo inatoa fursa ya usimamizi wa kodi wnye utaalamu kwa wadau wengine wanaohusika ili kuyafahamu Makubaliano ya Mfano ya Utozaji Kodi Mara Mbili;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

SASA LINAAZIMIA:

1. Kupitisha rasimu ya kwanza ya Makubaliano ya Mfano ya Utozaji Kodi Mara Mbili ya Umoja wa Afrika.
2. Kuiomba Kamati ya Fedha na Uongozi wa BA kuhakikisha uwasilishwaji wake kwa AUCIL kwa ajili ya kujadiliwa na baadaye kuwasilishwa kwa Vyombo vya Sera vya UA.
3. Kuipa madaraka Kamati ya Fedha iendelee kutekeleza kufanya shughuli za uelimishaji na kujenga uwezo kuhusu Makubaliano ya Utozaji Kodi Mara Mbili ya Umoja wa Afrika;
4. Kuwashukuru ATAF, AUCIL na AUC na washirika wengine kwa msaada uliopatikana wa kuandaa Makubaliano ya Mfano ya Utozaji Kodi Mara Mbili ya Umoja wa Afrika, na kuimarisha ushirikiano huo wa kushughulikia kodi na DTAs.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

**PAP.5/PLN/RES/5/OCT.19**

**AZIMIO KUHUSU KUSIMAMIA MADENI NA KUPAMBANA NA RUSHWA KATIKA AFRIKA**

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA** pia Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, inayolipa BA mamlaka ya kuwezesha utekelezaji wa sera, malengo na programu za Umoja wa Afrika na kusimamia utekelezaji wake mzuri;

**LIKIREJEA** Azimio Maalum la Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa UA kuhusu Usafirishaji Haramu wa Fedha kwenye Mkutano wa Kawaida wa Ishirini na Nne huko Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Januari 2015 na Mapendekezo ya Ripoti ya Jopo la Viongozi kuhusu Usafirishaji Haramu wa Fedha kutoka Afrika;

**LIKIREJEA PIA** Azimio la Kushinda Mapambano dhidi ya Rushwa: Njia Endelevu katika Mageuzi ya Afrika lililopitishwa na Bunge la Afrika tarehe 17 Mei 2017;

**LIKISIKITISHWA** na ukweli kwamba rushwa na usafirishaji haramu wa fedha vinatishia malengo yetu ya kukomesha umaskini na njaa katika Afrika na kufikia maendeleo endelevu katika vipengele vyake vitatu kupitia kuhimiza ukuaji jumuishi wa uchumi, kulinda mazingira na kuhimiza kuthamini makundi yote ya jamii, ahadi thabiti za kisiasa za kushughulikia changamoto zinazoletwa na rushwa na usafirishaji haramu wa fedha nje ya Afrika lazima kuongezwe;

**LIKISIKITISHWA PIA** kwamba usafirishaji haramu wa fedha unasababisha uhaba wa fedha zilizopo kwa Serikali kutumia katika maendeleo ya taifa, ambako kunasababisha ukopaji na kuongeza viwango vya madeni ya serikali kuu katika Afrika;

**LIKISIKITISHWA ZAIDI** kwamba ununuzi duni wa umma, kutokuwepo kwa uwazi na usimamizi mbaya wa kodi unaofanywa na Serikali umesababisha mapato kidogo na kuhitaji kukopa;

**LIKITAMBUA KWA MASIKITIKO** kwamba motisha na kutokuwa na ukomo katika kodi bila ya kupata kwanza idhini ya Bunge na ukosefu wa ufuatiliaji na tathmini katika hilo kunaziweka nchi katika hatari ya kupoteza mapato na kuongezeka uwezekano wao wa kuingia katika mikataba ya kulipa madeni;

**LIKITAMBUA PIA** jukumu muhimu la Kamati ya Ukaguzi na Hesabu za Umma katika kuyasaidia Mabunge kuzuia rushwa na IFFs, na katika kudhibiti madeni;

**LIKITAMBUA ZAIDI** kwamba Mabunge yanaweza kutumia madaraka yake ya usimamizi katika mzunguko wa bajeti, uwajibikaji kwa matumizi ya fedha za umma na uwakilishi

wa watu wa kuziwajibisha serikali kwa kulipa fedha za umma kama ilivyoamuliwa katika mpango wa bajeti, ikiwa ni pamoja na makubaliano katika deni la umma;

**LIKIZINGATIA** Azimio la Kampala la Kamati za Muungano wa Afrika wa Hesabu za Umma (AFROPAC) lililopitishwa tarehe 22 Novemba 2018;

**LIKITHAMINI** uwasilishaji wa kitaalamu uliofanywa na wawakilishi wa Muungano wa Taasisi za Ukaguzi za Nchi Zinazozungumza Kiingereza Afrika (AFROSAI-e), AFROPAC, Mtandao wa Wabunge wa Afrika wa Kupambana na Rushwa (APNAC), Shirika la Fedha Duniani (IMF), Jukwaa la Usimamizi wa Kodi Afrika (ATAF) na Bodi ya Kupambana na Rushwa ya Umoja wa Afrika (AU-ABC);

**LIKIDHAMIRIA** kuwezesha utekelezaji wa uamuzi wa UA wa kutokomeza rushwa na kuhimiza utamaduni wa uwazi na utawala bora kulingana na hati za kisheria na kisera zinazohusika za UA;

**LINASHAWISHIKA** kwamba kuanzishwa kwa muungano ndani ya Bunge la Afrika wa kusimamia madeni na kukomesha rushwa kutawapa Wabunge wa BA muundo na jukwaa linalofaa la kushughulikia kwa uendelevu na kuliweka suala la usimamizi wa madeni na ukomeshaji wa rushwa katika ya ajenda za juu za kisiasa na kisheria kwenye ngazi za taifa na bara;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. **KUHIMIZA** uridhiaji kwa wote, utumikaji katika nchi na utekelezaji wa mikataba ifuatayo ya Umoja wa Afrika inayohusiana na kupambana na rushwa:

    i. Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia & Kupambana na Rushwa;
    ii. Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala;
    iii. Protokali ya Mkataba Uliyoanzisha Umoja wa Afrika unaohusiana na Bunge la Afrika;
    iv. Protokali ya Marekebisho ya Mkataba wa Sheria za Mahakama ya Afrika na haki za Binadamu;

2. **KUJIHUSUSHA** na Mabunge ya Afrika ya Taifa na Kanda kwa ajili ya kutumia kikamilifu madaraka yake ya kutunga sheria katika kutunga au kurekebisha sera na sheria za taifa zinazohusiana na mapambano dhidi ya rushwa, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hakuna ufilisi wa mali bila ya kushtakiwa na kwamba sheria ya uhalifu

inahamisha wajibu wa kuthibitisha kutoka kwa mwendesha mashtaka kwenda kwa mtuhumiwa kwa suala la rushwa na IFFs;

3. **PIA KUJIHUSISHA** na Mabunge ya Taifa na Kanda ya Afrika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa jukumu lao la usimamizi, utungaji sheria na uwakilishi ili kuhakikisha usimamizi unaofaa wa madeni ya serikali na kuvunja mzunguko wa rushwa, hususan kupitia ufuatiliaji kwa wakati na usimamizi wa ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi na ukaguzi wa deni la serikali, mtiririko wa fedha, mapato na ununuzi.

4. **KUTETEA** kwa pamoja na Vyombo vya Sera vya UA kwa ajili ya uanzishaji au uimarishaji, pale inapofaa, wa taratibu na mikakati ya taifa na bara inayolenga katika usimamizi na upunguzaji unaofaa wa madeni katika Afrika, ikiwa ni pamoja na kuhimiza uwajibikaji, uwazi na ushiriki wa raia katika michakato inayoongoza katika kuweka mikataba ya madeni ya serikali;

5. **KUTETEA** kwa pamoja na Vyombo vya Sera vya UA na Nchi Wanachama kwa ajili ya kuimarisha madaraka, uhuru na kuwa na uwezo kwa taasisi zote za taifa na bara zenye madaraka yanayohusika ya kupambana na rushwa, hususan Kamati ya Ukaguzi na Hesabu za Umma, taasisi za Kupambana na Rushwa, taasisi za ukaguzi wa hesabu na mfumo wa sheria;

6. **KUSAIDIA** na **KUHIMIZA** wajibu wa mitandao ya Mabunge ya kupambana na rushwa, raia, vyombo vya habari na asasi za kiraia katika kuendeleza utamaduni wa uwazi, uadilifu na uwajibikaji, na katika kuzuia uhamishaji haramu wa fedha na madeni yasiyolipika;

7. **KUFANYA KAZI** na wabia wenye nia katika uoanishaji wa sheria na viwango vya taifa katika uwanja wa usimamizi wa madeni na mapambano dhidi ya rushwa, pamoja na kupitia uandaaji, upitishaji na ulinganishaji wa sheria za mfano za bara, makubaliano ya mfano ya utozaji kodi mara mbili na viwango vingine vya kisekta kwa ajili ya kutumika, kurekebishwa au kupitishwa na Nchi Wanachama wa UA;

8. Kwa mtazamo wa ushughulikiaji endelevu na kuliweka suala la usimamizi wa madeni na rushwa katika ajenda za juu za siasa na sheria za Afrika, **LINAANZISHA** Muungano wa Bunge la Afrika wa Kusimamia Madeni na Kupambana na Rushwa (PAPA-DMAC), ambao utaandaliwa na kusimamiwa kama ifuatavyo:

   (i) Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha, Kamati ya Ukaguzi na Hesabu za Umma na Kamati ya Sheria na Haki za Binadamu watakuwa wajumbe wa PAPA-DMAC, ili mradi kwamba Mbunge yeyote wa BA anayependelea kushughulikia usimamizi wa madeni na kupambana na rushwa katika Afrika anaweza kushiriki katika shughuli za PAPA-DMAC.

   (ii) PAPA-DMAC utakuwa na Kamati ya Utendaji, ambayo itaundwa na Weenyeviti wa Kamati ambazo zimetajwa katika Kifungu cha 7.1 na watakuwa chini ya usimamizi wa Uongozi wa BA.

(iii) Muundo na ufanyajikazi wa PAPA-DMAC utarekebishwa kulingana na vifungu vinavyohusika ambavyo vinatumika kwa Kamati za Kudumu zote za Bunge la Afrika.

9. **KUTOA SHUKRANI** kwa AFROPAC, AFROSAI, APNAC, ATAF, AU-ABC na IMF kwa kuendelea kusaidia na kutoa msaada wa kitaalamu kwa BA na KUELEZA nia yao ya kurasimisha na kuimarisha ushirikiano wa kimkakati uliopo na unaotarajiwa ili kuongeza msaada wa kitaalamu na kifedha kwa shughuli zake zinazohusiana na kukomesha mzunguko wa rushwa katika Afrika.

**Midrand, Afrika Kusini**
**17 Oktoba 2019**

**PAP.5/PLN/RES/6/OCT.19**

## AZIMIO KUHUSU HALI YA AMANI NA USALAMA BARANI AFRIKA

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Anzilishi ya Umoja wa Afrika uliyoanzisha Bunge la Afrika kuhakikisha " kufikia umoja kamili na mshikamano kati ya nchi za Afrika na watu wa Afrika, kuendeleza amani, usalama na utulivu barani na kuimarisha ushiriki katika mawanda yote ya shughuli za binadamu ili kuinua hali ya maisha ya watu wa Afrika ;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3 (a), (f), na (k) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika unaoeleza malengo ya Umoja ili kuwa na umoja na mshikamano mkubwa miongoni mwa nchi za Afrika na watu wa Afrika;

**LIKIZINGATIA PIA** bara ya 3 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoanzisha Jumuiya ya Uchumi Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika, linalowezesha utekelezaji bora wa sera na malengo ya Umoja wa Afrika ; ya kukuza kanuni za haki za binadamu na demokrasia Afrika ; na kukuza amani, usalama, na utulivu;

**LIKIREJELEA Ibara ya** 20 Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika na pia Ibara ya 9 ya Protokali ya Marekebisho na Mkataba Anzilishi wa 2003; na Ibara ya 2 ya Protokali ya 2002 inayohusiana na Kubuniwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kama "chombo cha kudumu cha kutoa maamuzi, usimamizi na usuluhishi wa migogoro';

**LIKIREJELEA** lengo la 4 la Ajenda 2063, ambalo linatazamia Muundo wa Amani na Usalama unaofanya kazi kamili (APSA) na kukuza amani, usalama, na utulivu;

**LIKIZINGATIA** kwamba Ibara ya 18 ya Protokali inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika inayofafanua uhusiano wa karibu wa kikazi na Bunge la Afrika katika kuendeleza amani, usalama na utulivu katika Afrika na kuliwajibisha kuwasilisha ripoti kwa Bunge la Afrika itakayoliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake yanayohusiana na kukuza amani, usalama na utulivu barani Afrika ;

**LIKIZINGATIA KWA MASIKITIKO** kuwa ugaidi na siasa kali zinaendelea kuzidishwa kwa kuenea, kusambaa na usafirishaji haramu wa bunduki na silaha nyepesi, inayotishia amani, usalama barani na kulemaza juhusi za kuimarisha viwangoi vya maisha ya watu wa Afrika ;

**LIKIKUMBUKA** kwamba bara la Afrika lina historia ndefu ya migogoro ya silaha na ahadi ya Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ya kukomesha mapigano kufikia 2020;

**LIKISHUKURU** juhudi na ushirikiano wa Baraza la Amani na Uslama na BA kukomesha migogoro barani Afrika;

**LIKISHAWISHIWA** kwamba changamoto za amani na usalama zinaweza kutatuliwa tu kupitia juhudi za vyombo vyote vya Umoja wa Afrika;

**KWA MUJIBU WA** ya Kanuni 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo pamoja na mambo mengine, inalipa BA madaraka ya kuandaa mijadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kutoa maazimio kuhusu malengo na juu ya masuala yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Kamati za Uchumi za Kanda, Nchi wanachama na vyombo na taasisi zao;

SASA LINAAZIMIA:

5. **KUUOMBA** Uongozi wa Bunge la Afrika kupitia kwa Rais wa BA, kushauriana na Baraza la Amani na Usalama kuboresha uhusiano na ushirikiano kuhusu masuala ya amani na usalama, ikiwa ni pamoja na kutekeleza misheni ya pamoja ya kutafuta ukweli wa mambo na Kamati ya Ushirikiano, Uhusiano wa Kimataifa na Usuluhishi wa Migogoro katika maeneo yenye migogoro;

6. **KUIOMBA PIA** Kamati ya Ushirikiano, Uhuhisiano wa Kimataifa na Usuluhishi wa Migogoro kutekeleza misheni huru ya kutafuta ukweli wa mambowa ili kuongeza uelewa wao kuhusu sababu za migogoro katika bara na kulitaarifu bunge ipasavyo.

7. **KUOMBA ZAIDI** Kamati ya Ushirikiano, Uhusiano wa Kimataifa na Usuluhishi wa Migogoro kutekeleza shughuli zinazolenga kuendeleza ukomeshaji wa mapigano na Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika;

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Oktoba 2019**

**PAP.5/PLN/RES/07/OCT.18**

AZIMIO KUHUSU AMANI NA USALAMA KATIKA SAHARA

BUNGE LA AFRIKA,

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika, ulioanzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kikamilifu wa watu wa Afrika katika maendeleo na utangamano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3(a) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoelezea malengo ya Umoja wa Afrika ili kuwa na umoja na mshikamano mkubwa miongoni mwa nchi za Afrika na watu wa Africa;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3 (f) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoelezea malengo ya Umoja wa Afrika ya kukuza amani, usalama, na utulivu katika bara;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3 (k) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoelezea malengo ya Umoja wa Afrika ya kukuza ushirikiano katika nyanja zote za shughuli za binadamu ili kuboresha viwango vya maisha vya watu wa Afrika;

**LIKISIKITISHWA** na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Eneo la SAHARA ambayo yameendelea kuathiri shughuli za kujiingizia kipato kwa watu wa eneo hilo;

**LIKISITISHWA PIA** na kupungua kwa rasilimali maji kutokana na viwango vya juu vya joto kwenye eneo hilo ambavyo vinaathiri mazingira;

**LIKISITISHWA PIA** na ukweli kwamba eneo hilo limekuwa likikabiliwa na mashambulizi ya kigaidi ya mara kwa mara yanayofanywa na AQIM na Boko Haram na makundi mengine ya kigaidi;

**LIKISIKITISHWA PIA** na idadi ya silaha ndogo ndogo zinazosambaa katika eneo hilo;
**LIKIELEZEA KUSIKITISHWA** na athari kwenye usalama na utulivu zinazotokana na kuzuka mara kwa mara kwa migogoro, ugaidi na siasa kali barani;

**LIKIELEZEA KUSIKITISHWA** na suala la uhamiaji haramu na hali mbaya ya kibinadamu hususani kwa wanawake na watoto;

**LIKIZINGATIA KWAMBA** Ajenda ya 2063 inalenga kuwa na Afrika yenye amani na usalama ambayo haina migogoro;

**LIKIZINGATIA** kwamba ifikapo mwaka 2020 bara la Afrika linatakiwa kukomesha mapigano;

**LIKITAMBUA** kwamba sababu zinazosababisha kukosekana kwa usalama kwenye eneo la SAHARA ni suala lenye utata na kuhusisha mambo mengi;

**LIKITHAMINI** juhudi zinazofanywa na serikali kwenye eneo la SAHARA;

**LIKITAMBUA PIA** jukumu linalotekelezwa na Baraza la Amani na Usalama katika Kanda hiyo;

**LIKISHAWISHIKA** kwamba wabunge wana jukumu la kutekeleza kwenye kuimarisha amani barani Afrika;

**KWA MUJIBU WA** ya Kanuni 5 ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo pamoja na mambo mengine, inalipa BA madaraka ya kuandaa mijadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kufanya Uamuzi katika jambo lolote linalohusiana na UA na vyombo vyake, RECs, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zake;

**SASA LINAAZIMIA:**

5. Kuunda tume ya pamoja ya BA ya kutafuta ukweli wa mambo kwenye eneo la SAHARA ili kuelewa masuala ya wakimbizi na ya kibinadamu kwenye eneo hilo na athari zake kwa amani, usalama na utulivu kwenye eneo hilo.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Oktoba 2019**

AZIMIO KUHUSIANA

NA MAJADILIANO JUU YA RIPOTI YA SHUGHULI ZA BUNGE LA AFRIKA

BUNGE LA AFRIKA,

**LIKIZINGATIA Ibara ya** 17 ya Sheria ya kuanzisha Umoja wa Afrika, ambayo inaanzisha Bunge la Afrika (BA) ili kuhakikisha kuwepo kwa ushiriki kamili wa wananchi wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa Bara hili;

**LIKIZINGATIA vile vile Ibara ya** 3 Protokali ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Afrika kwa namna Inavyohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni 4 (a) ya Kanuni za Taratibu za Bunge la Afrika, ambayo inaliba madara BA kuwezesha utekelezaji wa sera, malengo na programu za Umoja wa Afrika na kusimamia utekelezaji wake kamili.

**LIKIBAINI juu ya** Ripoti ya Shughuli za Bunge la Afrika kwa kipindi cha mwezi Mei - Septemba 2019 kama ilivyowasilishwa na Rais wa Bunge la Afrika, na mazungumzo ya wazi kuhusiana na ripotu hiyo;

**KWA MUJIBU WA KANUNI YA** 5(b), (c) na (d) ya Kanuni za Taratibu za Bunge la Afrika zinazolipa madaraka BA miongoni mwa mambo mengine, kuandaa mijadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio juu ya malengo na kwa jambo jengine lolote lile linalohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vhake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo vyao na asasi zao;

SASA LINAAZIMIA:

1. **KUIPITISHA** Ripoti ya Shughuli za Bunge la Afrika kwa kipindi cha nwezi Mei _ Septemba 2019;

2. **LINAMTAKA** Rais na Uongozi wa Bunge la Afrika kufanya mazungumzo na Umoja wa Afrika, na hasa PRC juu ya kuwepo kwa mahusiano mazuri zaidi ya kikazi kwa madhumuni ya kuishughulikia bajeti ya Bunge la Afrika na changamoto ambazo Bunge la Afrika inazikabili kwa sababu ya kupunguzwa kwa bajeti yake ya mwaka 2019;

3. **LINAZIDI KUUTAKA** Uongozi wa Bunge la Afrika kufanya mazungumzo na vyombo vya sera vya Umoja wa Afrika kurudisha maslahi na posho za Wabunge wa Bunge la Afrika ili waweze kufanya kazi na shughuli zao vizuri zaidi.

4. **LINAUKUMBUSHA** Uongozi wa Bunge kuhakikisha kuwa Kamati za Kudumu zinapatiwa msaada unaohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya shugfhuli zao;

5. **LINAUPONGEZA** Uongozi wa Bunge na Seketeriati kwa kuboresha hali ya kufanyakazi ya Wabunge wa Umoja wa Afrika hasa kuhusiana na vifaa vya tafsiri na utayarishaji wa nyaraka

**Limepitishwa Midrand, Afrika ya Kusini**
**17 Oktoba 2019**

## AZIMIO KUHUSU RIPOTI YA MWISHO YA KAMATI YA UKAGUZI WA HESABU ZA UMMA YA BUNGE LA AFRIKA

**BUNGE LA AFRIKA**,

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika (BA) ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA PIA** bara ya 3 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoanzisha Jumuiya ya Uchumi Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya kanuni za utaratibu za Bunge la Afrika, linalilipa BA mamlaka ya kuwezesha utekelezaji bora wa sera na malengo na Programu za Umoja wa Afrika na kufuatilia utekelezaji kamili;

**LIKIZINGATIA** ripoti ya mwisho ya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma, Oktoba 2019, ikiwa ni pamoja na mapendekezo yaliyomo, ikijumuisha maoni yaliyotolewa na wabunge wa BA wakati wa kikao cha pamoja;

**LIKIZINGATIA KWA MAKINI** kuyumbayumba kwa cheo cha Katibu, nafasi katika Ofisi ya Katibu na hitaji la Sekretarieri huru inayozingatia Kanuni 17 na 21 ya Kanuni za Utaratibu ya Bunge la Afrika pamoja na uhisiano katii ya Uongozi wa Bubge na Ofisi ya Katibu wa Bunge;

**LIKIZINGATIA KWA MAKINI PIA** kuzidi kutotekeleza mapendekezo mengi ya ukaguzi wa hesabu yaliyotolewa na wakaguzi wa nje wa hesabu, Bodi ya UA ya Wakaguzi wa Nje pamoja na Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma;

**KWA MUJIBU WA** ya Kanuni 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo pamoja na mambo mengine, inalipa BA madaraka ya kuandaa mijadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kutoa maazimio kuhusu malengo na juu ya masuala yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Kamati za Uchumi za Kanda, Nchi wanachama na vyombo na taasisi zao;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. **KUPITISHA** ripoti ya mwisho ya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma, Oktoba 2019 pamoja na mapendekezo yaliyomo;

2. KUTOA MAAGIZO kwa Sekretarieti kutekeleza kikamilifu Kamati ya Mchakato wa ukaguzi wa ndani ambayo itashirikisha na Wakuu wote wa Vitengo kuwezesha na kuhakikisha utekelezwaji wa wakati wote wa mapendekezo yote ya ukaguzi na CAPA na pia kuwezesha ukaguzi wa kishirika wa BA ufanyike chini ya usimamizi wa CAPA;

3. **KUHIMIZA** Uongozi wa Bunge la Afrika kuhakikisha kuwa watu waliohitimu kitaaluma wangeajiriwa kwenye nafasi zilizowazi kwa usimamizi unaofaa na bora wa Secretariati;

4. **KUHIMIZA ZAIDI** Uongozi wa Bunge la Afrika kushughulikiwa masuala yanayohusu idadi kubwa ya watu kuondolewa kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kuharakisha kuajiriwa kwa Katibu kuhakikisha utulivu na kutoa mwongozo makakati na uratibu kwa wafanyakazi, idara kwa uendeshaji bora wa BA;

5. **KUZINGATIA** kurekebishwa kwa Kanuni ya 17 (a & b) ya Kanuni za BA za Utaratibu zinazohusiana na masuala ya usimamizi na utawala na majengo ya;

6. **KUHIMIZA** Uongozi wa Bunge kuvikumbusha vyombo vya sera vya UA kuchukua hatua za kuharakisha marekebisho ya nyongeza za makubaliano kwenye Makubaliano ya Uwenyeji kati ya UA na Afrika Kusini kuhusiana na;

7. **KUOMBA** Uongozi wa Buge kuhakikisha kwamba mapendekezo yote ya ukaguzi wa hesabu yanazingatiwa ili taswira ya Bunge la Afrika iweze kuboreka kwa Vyombo vya Sera ya AU;

8. **KUOMBA PIA** Uongozi wa Bunge kuchukua hatua muhimu za kushughulikia masuala yanayohusu kutotekelezwa kwa mapendekezo ya ukaguzi wa hesabu na utekelezaji wa bajeti ili kuepuka vikwazo kutoka kwa UA;

9. **KUOMBA PIA** Uongozi wa Bunge kushirikiana na Vyombo vya Sera ya UA kupata 50% iliyokataliwa katika bajeti ya bima ya matibabu ya Wabunge imerejeshwa na kuhakikisha kwamba kanuni, sheria na sera za UA zinatoa faida na haki ya "Maafisa Waliochaguliwa", ikiwa ni pamoja na faida za kusafiri katika ndege katika daraja fulani na marupurupu;

10. **KUOMBA** Uongozi wa Bunge kuwajibisha mmoja kwa mmoja au kwa pamoja watu waliokuwa wanasimamia Mfuko wa BA uliokuwa na USD 140, 143.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

**AZIMIO LA KUMUENZI MHESHIMIWA ROBERT GABRIEL MUGABE, ALIYEKUWA RAIS WA JAMHURI YA ZIMBABWE**

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika, ulioanzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kikamilifu wa watu wa Afrika katika maendeleo na utangamano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA PIA** bara ya 3 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika inayoanzisha Jumuiya ya Uchumi Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya kanuni za utaratibu za Bunge la Afrika, linalowezesha utekelezaji bora wa sera na malengo ya Umoja wa Afrika;

LIKIKUMBUKA kwamba aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, Mhe. Robert Gabriel Mugabe, mwana halisi wa Afrika, aliyeitetea nchi yake na Afrika duniani kote;

LIKIKUMBUKA PIA jitihada zake kuhusu kuheshimiwa kwa Afrika na nchi za Afrika kutendewa kwa usawa katika jumuiya ya kimataifa;

LIKIKUMBUKA ZAIDI dhamira yake ya kukuza na kulinda haki za msingi za wanawake, vijana na watoto;

LIKITAMBUA utetezi wake wa wanawake, kama washirika muhimu wa maendeleo barani Afrika;

LIKITAMBUA PIA urithi aliyouacha sio tu kwa Zimbabwe na Afrika bali pia kwa dunia nzima;

LIKITAMBUA ZAIDI mafundisho muhimu kutoka kwake kuhusiana na mshikamano na ushirikiano kwa ajili ya Afrika;

LIKITAMBUA PIA nia na dhamira ya dhati ya Mhe. Robert Gabriel Mugabe katika kuhakikisha kuwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika inajitegemea kifedha ili kuliwezesha bara la Afrika kuwa na umiliki wa programu zake;

**KWA MUJIBU WA** ya Kanuni 5 (b), (c) na (d)ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo pamoja na mambo mengine, inalipa BA madaraka ya kuandaa mijadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kutoa maazimio kuhusu malengo na juu ya masuala yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Kamati za Uchumi za Kanda, Nchi wanachama na vyombo na taasisi zao;

LINAAZIMIA :

1. Kuungana na viongozi wa Afrika, watu wa Zimbabwe, Waafrika na watu wengine duniani kumuenzi inavyostahili shujaa huyo aliyefariki akiwa na umri wa miaka tisini na mitano.

2. Kukipa chumba cha Kamati namba tatu jina la aliyekuwa Rais, Mhe. Robert Mugabe

Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini
Tarehe 17 Oktoba 2019